es Salaam ambapo kwa sasa kuna idadi kubwa zaidi hatua inayotokana ushawishi wa Tasac katika kuzivutia meli hizo.

kahawa yote iliyozalishwa na wakulima nchini kiasi cha tani 59,318 imepata soko nje ya nchi ambayo wastani wa kilo moja ya kahawa iliyobangukiwa maganda

kwa wingi kwani soko lipo na bei ni nzuri.

"Soko la kahawa limerudi,utaona kahawa yote tani zaidi la 59,000 tuliyozalisha hapa nchini

wanategemea kuvuna tani zaidi ya 70,000 za kahawa kutokana na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa yenye mvua ya kutosha.

Akizungumzia mikakati

kusambaza miche bora ya kahawa kwenye mikoa ya Mogorogo,Geita na Iringa na kwamba lengo lao ni kusambaza jumla ya miche bora 6,000,0000.

kujitafutia kipato na kuweza kujikikimu kimaisha.

Alibainisha changamoto mojawapo kuwa ni masoko ambapo kwa kutumia mitandao watu wengi wamekuwa matapeli.

HABARI LEO UK 7.

# *Samaki 'kaa mwizi' awa kivutio Sabasaba*

**Na Ikunda Erick**

JAMII ya samaki kaa aitwaye Tuyuli au kaa mwizi kutokana na tabia yake ya kuiba nazi kwenye minazi, amekuwa kivutio kwa wananchi katika Maonesho ya 44 ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere.

Akimzungumzia kaa huyo katika banda la Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu(MPRU), Mhifadhi Utalii, Davis Mpotwa alisema jamii hiyo ya kaa aitwaye Tuyuli ni moja ya viumbe baharini vilivyo kwenye hatari ya kutoweka kutokana na wavuvi na watu kuwaua kupata kitoweo na wengine kuona ni viumbe waharibifu.

"Tuyuli tumemleta sabasaba kwa mara ya kwanza amekuwa kivutio kwa wananchi wanaotembelea maonesho haya, kwanza ni jamii ya kaa asiyejua kuogelea na anaishi kwenye mapango maeneo ya pwani chakula chake ni nazi, na vitu vingine lakini pia akikuta chakula au ugali anaiba anakula",alisema Mpotwa.

Alisema Tuyuli ni jamii ya kaa ana uwezo wa kuwa mrefu hadi futi tatu na uzito wa kilogramu nne hadi tano na anaishi miaka 60 lakini pia anataga mayai zaidi ya 500 lakini yanayoanguliwa ni machache kutokana na tabia yake ya kutotulia hivyo kufanya samaki kuyala na mengine kuharibika.

Mpotwe alisema baada ya mayai yake kuanguliwa watoto wake huvaa magamba ya konokono kwa ajili ya kujilinda kwa sababu ngozi zao ni laini na wakianza kuwa wakubwa hujivua gamba na kuendelea na maisha yao kwani huwa na uwezo wa kujilinda wenyewe.

Alisema Tuyuli hajui kuogelea tofauti na kaa wengine na kwamba huishi zaidi maeneo ya Pwani kwenye mapango na hupenda zaidi kutembea na kula usiku kwa kupanda minazi kula nazi hivyo wananchi wa Pwani huwaua zaidi kwa kuwa wanasema ni waharibifu.

"Hawa Tuyuli ni viumbe waliohatariki kupotea, wanapatikana maeneo machache sana duniani ikiwemo Tanzania na hata hapa nchini wanaonekana zaidi kwenye Kisiwa cha Mbudya,Dar es Salaam ambacho bado kiko salama hakijaaribiwa,"alisema Mpotwa. Alisema uwezo wa Tuyuli kukaa majini ni saa moja kisha anatoka na kwenda nchi kavu na kwenye mapango kutafuta malisho ikiwemo kupanda kwenye miti ya minazi kula nazi.

Scanned with CamScanner

nao weweze kunufaika, alieleza Kiswaga.

Awali Afisa Ushirika Wilaya ya Bariadi, Lucas Kiondere alisema kuwa, jumla ya vyama vya Msingi

kilo chache anashindwa kuweka fedha zake benki kwa sababu nauli atakayoitumia ni zaidi ya ile anayoifuata,"alieleza Mzee Nkenyenge.

MAJIRA UK 5

# Serikali kujenga kituo kikubwa cha ukuzaji viumbemaji Chato

changamoto ya uhaba wa samaki ulioanza kujitokeza kwenye vyanzo vya asili.

"Kituo hiki kitahudumia mikoa yote inayozunguka kanda ya ziwa na maeneo ya jirani na ukanda huu na tutawafundisha wafugaji samaki, maofisa ugani wa fani ya ufugaji wa samaki, pia kitatumika kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wanaosoma katika ngazi mbalimbali huko vyuoni,"alisema Madala.

Dkt Madala aliongeza kuwa kituo hicho kitakuwa kama cha mfano na kitawasaidia kutoa muongozo wa kujenga vituo vingine katika maeneo yanayozunguka Ziwa Tanganyika, Nyasa na maeneo ya Pwani lengo likiwa ni kuhakikisha viwanda vyote vya samaki havikosi malighafi ili kufikia adhima ya kuwa nchi ya viwanda.

Mapema Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho aliishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kupeleka mradi huo katika wilaya hiyo na aliahidi kufuatilia kwa ukaribu hatua zote za ujenzi wa kituo hicho hadi kitakapokamilika.

Naye, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Rubambangwe, Restituta Majura alisema kuwa mradi huo ukikamilika utawanufaisha sana wakazi wa kijiji hicho kwani utatoa ajira kwa wananchi na kusaidia kuchachua uchumi wao.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA RUNGWE LILILOKO TUKUYU**
**KESI NA. 15/2019**

**(SHERIA YA USAJILI WA ARDHI (SURA 334) KUPOTEA KWA HATI ZA KUMILIKI ARDHI**

**HATI NA:** 425
**MMILIKI ALIYESAJILIWA:** MICHAEL

NIPASHE UK 17.



Mfugaji wa kuku, Bahati Issa mkazi wa Kijiji cha Kikungwi, Kusini Unguja akiihudumia mifugo yake jana. Ufugaji wa kuku ni moja ya nyenzo ya kuwakomboa wanawake kiuchumi visiwani Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**